

SEMINA YA UTAWALA BORA KWA MADIWANI.

Madiwani wa halmashauri ya wilaya ya Mpanda pamoja na Nsimbo wamepatiwa semina elekezi ya namna ya kusimamia sheria, taratibu na kanuni. Mafunzo hayo yamefanyika Januari 21-23, 2016 katika ukumbi wa halmashauri ya wilaya ya Mpanda-Idara ya maji. Mafunzo ya utawala bora kwa madiwani na wataalam yametolewa na shirika la TUUNGANE kwa kushirikiana na Taasisi ya Jane Goodall.

Lengo kuu la mafunzo hayo ya utawala bora kwa madiwani na wataalam ni kuwajengea uwezo wa kujielewa na kuelewa majukumu yao wakiwa viongozi. Diwani ni “MWAKILISHI” wa watu na wala siyo mjumbe au mwajiriwa wa halmashauri. Naye mkuu wa wilaya ya Tanganyika Salehe Mhando amesema, *“Diwani anapaswa aelewe mamlaka yake ni yapi, matarajio ya jamii alimotokea na matakwa ya makundi mbali mbali wanaoishi katika kata yake”*. Maisha ni siasa ila tunahitaji siasa safi na siyo siasa uchwara.

Madiwani wanapaswa kuelewa kuwa, Kuongoza ni kuonesha njia, kutangulia na kuelekeza katika upangaji, utekelezaji na usimamizi wa majukumu ya umma. Naye muwezeshaji kutoka taasisi ya Jane Goodall Theo Macha amesema, *“Kuongoza ni kujenga moyo wa pamoja miongoni mwa wanaongozwa na kuwahamasisha ili watekeleze yale yaliyokusudiwa. Ili kiongozi aongoze, lazima apate wafuasi ambao wanamkubali na kumfuata. Ni jukumu la kiongozi kujenga mazingira mazuri mahali pake ili kuhakikisha kuwa anakubalika. Kuongoza ni tendo linalohitaji maarifa na ujuzi ambao mtu anaweza kujifunza. Kwa msingi huu, uwezo wa kuongoza ni kipaji, pia linaweza kuletwa kwa kujifunza”*.

Wajibu mkubwa kwa diwani kama kiongozi, anatakiwa kuhakikisha kata yake inakuwa mfano wa kuigwa kwa kuwa na maendeleo mazuri. Katika halmashauri ya wilaya ya Mpanda kuna changamoto ya upungufu wa vyumba vya madarasa kwa shule za msingi, utoro wa wanafunzi, migogoro ya matumizi bora ya ardhi na utunzaji mazingira kwa ujumla. Kila diwani anatakiwa kuhakikisha wanafunzi wanaotoka katika eneo lake wanasomea darasani, wanapata chakula cha mchana na kuhudhulia masomo yao muda wote.

Kiongozi inatakiwa awe msitari wa mbele katika kuchangia maendeleo kwa wananchi wake na kuwa mfano wa kuigwa. Wananchi wanategemea diwani awape mawazo na njia sahihi ya utatuzi wa shida au matatizo yanayowakabili. Diwani kama kiongozi, hatakiwa kuwa chanzo cha kuvunja sheria, kanuni na taratibu za serikali kwa kusema, *“waache wapiga kula wangu”* wakati wataalam wanapotekeleza majukumu yao.

Naye Mkurugezi msaidizi wa taasisi ya Jane Goodall Mary Mavanza amefafanua kuwa, *“Utawala Bora ni mfumo wa utawala unaohusisha jamii yake kama muhusika mkuu katika kusimamia matumizi ya rasilimali zake kwa manufaa yake”*. Misingi na sifa za Utawala Bora unazingatia; Demokrasia, ushirikishwaji, utawala wa sheria, uwazi, uwajibikaji, haki, usawa na uadilifu. Diwani anatakiwa awe mtetezi wa haki za kila mwananchi bila kujali tofauti za itikadi, dini, rangi, jinsia na chama cha siasa.

Katika uendeshaji wa ofisi za serikali za mitaa, Mkurugenzi ndiye mtendaji Mkuu na Afisa Masuuli wa halmashauri. Shughuli zinazotekelezwa na watendaji wa serikali za mitaa lazima zitokane na maamuzi ya vikao vya halmashauri. Maamuzi ya vikao vya halmashauri yanarekodiwa na karani wa halmashauri kwenye daftari maalumu la kudumu. Daftari la mhitasari hutumika kama rejea katika ufuatiliaji wa

utekelezaji wa maamuzi ya halmashauri. Kumbukumbu hizo huthibitishwa na wajumbe wa mkutano kwenye kikao kinachofuata na kusainiwa.